**Mapendekezo “Kumi Bora” Kuhusu Kazi Ya Huduma.**

Ni agizo kuu ajabu Bwana alilopata kumpatia mwanadamu. Agizo ambalo hata hivyo alilielewa na kulifanya! Hakuacha “fahari yote ya mbinguni, akijua hatima yake?” Akijua kwamba atafanyika mdogo kuliko malaika, Waebrania 2:5-9. Akijua kwamba atavaa umbile la mwanadamu. Akijua kwamba ili kufanya hivyo, angelazimika kutohesabu ubora wake kama kitu cha kushikamana nacho, Wafilipi 2:6. Hata hivyo, bado alikuja, “kutafuta na kuokoa kilichopotea,” Luka 19:10.

Yesu akafanyika kuwa dhabihu tuliyoihitaji, Waebrania 9:14. Na sasa anatutaka sisi tuwe na nia iyo hiyo (Wafilipi 2:5) na kujitoa mhanga, kwa ajili ya nafsi za wanadamu. Ndiyo, sisi ni wanadamu, Ndiyo, tunajua dhambi ni kitu ni nini. Ndiyo, wote tuna mapungufu fulani fulani. Na Mungu akipenda, tunayafanyia kazi hayo mapungufu na kuyageuza kuwa matunda kwa ajili ya Mwokozi wetu. Walakini katika Wafilipi 2 siyo tu kwamba tumepewa kielelezo kamili cha Yesu Kristo katika kujidhili. Pia sura hiyo hiyo inatufundisha kwamba hatuhitaji kuwa Kristo ili kujitolea kuwa wahanga kwa ajili ya Mungu (Warumi 12:1). Mstari wa 19-30 inaonyesha watu wawili, Timotheo na Epafradito, waliojitolea kuwa wahanga kwa ajili ya kazi ya Bwana wetu Yesu Kristo. Watu hawa wa kawaida kabisa, kama tulivyo sisi na matatizo ya kawaida, ambao walikabiliwa na kuumwa karibia kufa, waliugua, na kuwa na matatizo binafsi na yale yatokanayo na hisia, Wafilipi 2:26-27; 1 Timotheo 5:23; 2 Timotheo 1:7.  Pamoja na matatizo hayo yote, bado “walifanya kazi ya Kristo,” (2:30) Hawakuzijali nafsi zao kwa ajili ya kuwatumikia wengine.

Leo, tunao waume kwa wanawake walio hodari kwenye katika kazi ya huduma. Watu waliojitoa mhanga kwa ajili ya waliopotea. Wako wengi, wahenga wasioimbwa miongoni mwetu leo ambao waliyahatirisha maisha yao hadi kulifikia kabila la mbali kabisa. Hata sisi wakati fulani, tunapaswa tuwekwe kwenye kumbukumbu ya mambo fulani fulani. Kwa sababu hiyo, hebu tufakari yafuatayo.

1) Kutafuta hela kwa ajili ya huduma ni kazi ngumu. Ni sawa na kukamua maziwa kutoka kwenye chuchu zilizokaukiana. Na bado, tulimkuta mjane na senti yake. Wakati wangu nilikutana nao wengi. Na ninamshukuru Mungu kwa kuniwezesha kukutana na kunifanya nishuhudie watu waliotoa namna hii. Kama Wamishonari, tunatakiwa kukumbushwa kwamba tunaishi kwa upendo wa matoleo ya wajane hawa na wengineo. Ndiyo, tuna haki ya “kula na kunywa,” 1 Wakorintho 9:4. Tuna haki ya kupata “riziki kwa hiyo injili,” 1 Wakorintho 9:14. Lakini, hatuna haki ya kujaza vihenge vyetu kwa senti ya mjane.
    - A) Tunapozungumzia kutafuta  hela za kuendeshea kazi ya huduma, Usipitilize mpaka! Uwe mkweli, mwaminifu ukiwa umejaa uadilifu
    - B) Kutafuta hela za kuendeshea huduma ni kazi ngumu. Na kutenda dhambi ili upate hela za kuendeshea huduma bado ni dhambi, Warumi 3:8.
        1. Watafuta hela za huduma –Njia nzuri ya kutafuta hela za huduma ni hii; Amini kwamba Mungu atakupa. Kumbuka Mwanzo 22:14- Yehova Yire. Fanya kazi, fanya kazi, na fanya kazi!
        2. “Mapema asubuhi hii ulipotoka chumbani, ulifikiria kuomba?” – Omba, na ongeza tena kuomba!
2) Jinsi ya kutumika vilivyo-Paulo akawa “ mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi ,” 1 Wakorintho 9:19. Kiujumula Yesu ndiye kilelezo kamili, na anatuonyesha ya kuwa ili kutumika kwa ufanisi na vilivyo, tunalazimika kujichanganya na watu. Ndiyo, kuna wakati wa kuandaa/kutoa hotuba na muda wa mafunzo ya uhubiri . Pia kuna wakati wa kutembea kwa

miguu na kuwafikia wanaolia na kuwakuta watafutao, na wale waioacha kulia kitambo. Siku zote nakumbuka maagizo ya Paulo kwetu katika 1 Wakorintho 4:1. Tu wahudumu-“wa kujidhili,” na mawakili-“msimamizi wa watumwa.” La msingi hapa ni kwamba ili kuweza kufanikiwa vilivyo, ni lazima ujifunze kuongoza na kutumika wakati huo huo. Kwenda katika eneo la kazi katika nchi ya ugenini na kukaa ofisini na kuelekeza wengine kwa kwenda, tabia hiyo haitakufanya uwe askari bora kwa ajili ya Kristo kama ikupasavyo. Kiongozi bora ni Yule anayejijumuisha na wengine!

3) Uweza uokoao-Ndugu, kumbukeni uweza wa kuokoa ulio katika Injili, Warumi 1:16. Kumbukeni kwamba ni upanga wenye makali yakatao kuwili; Wabrania 4:12. Ikiwa imeletwa ili kuchoma na kupenya, Matendo ya mitume 2:37; 7:54; 9:5, na kumwingiza mtu katika uliwengu wa waliokombolewa. Ingawaje wengi wetu tunafanya kazi katika nchi masikini, hatupo kwa ajili ya kununua roho za watu kwa kima cha dola za kimarekani. Kima pekee cha kuweza kuokoa roho za watu ni damu ya Kristo. Kuingia tu kwenye maji, haimaanishi kuwa mtu ametakaswa na kusafishwa. Neno la Mungu ndilo litakasalo na kusafisha, Waefeso 5:26. Na tusisahau ukweli huu.

Sasa, sipingamani na matendo mema ( kusaidia). Baada ya kutoa hotuba mlimani (Mathayo 5-7), Yesu aliendа kutenda mema (Mathayo 8), nasi vivyo hivyo tunapaswa kufanya. Hata hivyo, ni vyepesi kwetu sisi kutingwa na kutenda mema na kusahau kuhuburi maneno yawezayo kumweka mtu huru! Ni jambo zuri kama unaweza kuwaponya watu 20,000 kwa mwaka. Hata hivyo, bado kama hao 20,000 na familia zao, hawakupata kusikia habari njema za Bwana Yesu, Ni nini basi?

4) Mafundisho- Bwana yuko wazi kabisa kwamba pando asilolipanda litangolewa, Mathayo 15:13. Miaka michache tu baada ya maneno hayo kusemwa, Roho Mtakatifu aliandikia kwamba shetani na vikosi vyake vya mapepo atamshawishi mtu kwa kutumia mafundisho ya uongo, 1 Timotheo 4:1. Mungu ametukirimia vitu vyote vitupasayo uzima na utauwa, 2 Petro 1:3. Ametupatia kila kitu tunachohitaji ili kuwa watimilifu, 2 Timotheo 3:16-17. Na sasa leo tunatakiwa kulipokea kama lilivyoandikwa kwa maana litaokoa roho zetu, Yakobo 1:21. Sheria timilifu ya uhuru, Yakobo 2:25! Najua inaumiza kuona maelfu wanapotea dhambini, na kwenda motoni kwa sababu hawataitii injili. Lakini uhalisia hautupi haki ya kuomba radhi kwa kutoitii kweli. Na wala uhalisia hautupi haki ya kuulowesha upanga wa roho, ukatao kuwili ambao huchoma na kugeugeuza kuwa peremende ya pamba. Injili iliyookoa mnamo karne ya kwanza-Huokoa na leo, Petro 1:22-25.

5) Mchezo wa idadi – Ni hakika kwamba watu wanajali idadi. Hivi ndivyo wanavyoelewa na kuchukulia mambo. Na kwa sababu hiyo, wamishonari wanakumbwa na shinikizo ili kufikia idadi fulani. Tunachotakiwa kuelewa ni kwamba Kristo hakufa kwa ajili ya idadi. Alikufa kwa ajili ya wote. Na Wamishonari wengi wanafanya kazi mchana na usiku, kama Paulo katika 1 Wathesalonike 2:9. Na tunawashukuru kwa dhabihu hiyo. Yafuatayo ni mambo muhimu kuhusiana na mchezo wa idadi.

a. Mungu anawataka mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Watu wengine watachukua muda kuelewa injili kuliko wengine, Lakini kwa ajili ya kufikia idadi, hatuwezi kuachana nao wale wanaoonekana vichwa ngumu, kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yao pia. Namfikiria Paulo, hakuwa kichwa ngumu hata kidogo? Kama aliwatokea watu 5, 000 siku ile, angewashawishi wote wabatizwe. Lakini bado aliondoka peke yake!

b. Kamwe tusipotoshe idadi. Iko hivyo ilivyo, ni uongo! Mashinikizo ya nyumbani hayatahalalisha kosa.

c. Makusanyiko fadhili lazima yaelewe kuwa maeneo mengine ni rahisi kufanya kazi kuliko mengine. Kwa kubatiza watu wengi Tanzania ukilinganisha na ilivyo Scotland, haimaanishi kwamba Yesu hawajali wale watu wa Scotland. Nasi tunatakiwa kuhakikisha kuwa Ulimwengu wote unasikia ujumbe wa Mungu.

6) Safari za kazi ya huduma:

a) Safari fupi za kazi ya huduma huweza kuwa nyenzo nzuri au huweza kuwa chanzo cha uharibifu.

Mambo machache ya kuzingatia: 1-Safari fupi za huduma hazijakusudiwa wala hazijatazamiwa kuwa likizo.  Ingawaje, watu wengi huchukua likizo na kutumia muda huo ili kumtumikia Mungu katika safari fupi za kazi ya huduma, hilo ni jambo jema na la kupongezwa. Walakini, kama tunapata fedha kutoka katika kanisa, kutoka kwa wajane, kutoka kwa mtu yeyote-kwa jina la safari fupi za kazi ya huduma. Basi hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Kama unataka likizo, basi chukua likizo. Lakini siyo kwa gharama ya Kanisa. 2- Kila uendako, wewe ni mgeni. Kwa hiyo, uwaheshimu wenyeji, uwaheshimu wamishonari weneyeji, na ufanye kazi kwa bidii. 3- Usiwaahidi wenyeji kitu ambacho hutatimiza. Jambo hili hugeuka kuwa kero kwa Mishonari mwenyeji mara uondokapo. 4- Usitumie muda wako kuhukumu kazi unayosaidia. Upo kwa juma moja au mawili. Na ingawaje upo kwa muda mfupi, hutaweza kujua kinachoendelea nyuma ya pazia, mwachie mishonari mweneyeji.

b) Kuwa mishonari wa kudumu ni changamoto. Wengine hufanya kazi usiku na mchana ili kuokoa roho za watu. Na wengine hujitaabisha hadi kufikia hatua ya kufa kama Epafradito. Kumbuka, tunaenda kufanya kazi, kutumika na kuokoa. Hakuna kucheza, likizo na kuwinda. Tatizo sio kupumzika au likizo. Yesu alikuwa akiondoka na wachache kwenda Kanaani ili kupata mapumziko mafupi. Hata hivyo, Wamishonari hawajatumwa kwenda kwenye “maadhimisho matukufu.”  Wazee na Wamishonari lazima wafanye kazi kwa uwiano sawa ili kuhakikisha kuwa jambo hili halitokei.

7) Wamishonari na  Mafundisho-Iweni waadilifu! Usije Marekani kutafuta pesa na kujifanya kimafundisho u wa namna ambayo kiuhalisia siyo. Huko ni kuwa ndumila kuwili, na kama Yakobo asemavyo katika Yakobo 1:8, “Mtu wa nia mbili husita-sita katika njia zake zote.” Ni lazima tutambue kuwa kweli ya Mungu haibadiliki ghafla, na wala haibadiliki tunapovuka mipaka (1 Pet. 1:22-25).

8) Tumika usijifanye Bwana-Ninyi ni watumishi wa Aliye juu. Ni jina lake ndilo tunalotakiwa kulitukuza. Na tunafanya hivyo kwa utumishi, kazi, damu na machozi yetu! Hivyo, kama vile Petro alivyowaelekeza wazee, katika 1 Pet. 5:1-3, tusijifanye mabwana juu yao tunaowatumikia. Na tukumbuke kuwa sisi hatuna ubora wowote kuwazidi tunaowatumikia. Tusijivune, 1 Wakor. 4:18. Na tuwe pamoja kuwatumikia wengine, 1 Wakor. 9:22. "Vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa." 1 Wakor. 10:33.

9) Utamaduni-Kila tuendako utamaduni unatofautiana, ni kama muda wote navuka mto mwekundu! Na kila mtu katika kila taifa hudhani kuwa utamaduni wake ni bora kuliko uwao wote duniani, na kila mtu lazima aige. Kama tunataka kufanikiwa katika kazi ya umishonari, bado tunatakiwa kujifunza utamaduni wa kila kabila tunalojitahidi kulifikia na kufanya kila tuwezalo kuuheshimu utamaduni huo. Yakiwa yamesemwa hayo, kama utamaduni unapingamana na Mungu, hapo tunatakiwa kumchagua Mungu kuliko mwanadamu, Matendo 4:19-20; 5:29. Na kamwe, hatutathubutu kuongeza au kubatilisha maneno ya Mungu ili kuhalalisha dhambi inayokubaliwa na utamaduni husika, Mathayo 15:1-13.

10) Lugha –Hakuna ushahidi wa upendo ulio mkuu kwa watu unaojaribu kuwaongoa kupita kujifunza lugha yao. Huendi kuwageuza wawe Wamarekani! Au kuwafanya wawe wa kizungu. Ingawaje kufundisha Lugha ya kiingereza ni njia nzuri ili kuwaokoa wengine, Si kila mtu anashawishika kuwa anahitaji kujifunza kiingereza. Njia bora ya kuthibitisha kuwa unawajali ni kuweza kuwafundisha neno la Mungu kwa lugha yao. Angalizo;

a) Ndiyo, unaweza kufanya makosa mawili matatu unapojifunza lugha, lakini watazidi kukupenda kwa kujaribu. Watakucheka. Lakini si kicheko cha kufanya duni, ni namna ya kukupongeza na kukuheshimu kwamba angalau unajaribu.
b) Ukijifunza lugha, unaweza kujua wanapokusema, na wanapokufanya mpumbavu.
c) Wakalimani ni wanadamu!!!!!! Huwa wanakosea!!!! Na njia pekee ya kuhakikisha kuwa ulichosema ndicho kinachosemwa, ni kujifunza lugha na kuisema mwenyewe!
d) Wakati fulani wakalimani hawawezi kukubaliana na ulichosema, na kwa makusudi wanasema wanachokitaka wao!
e) Wakati fulani wakalimani ni wahuni. Wakati kila kitu kimesemwa na kuisha, kama ukiwa msikilizaji na unajua lugha zote mbili, unakuwa umesikiliza hotuba mbili!
f) Siku moja nilisikia jambo moja la maana kuhusiana na hili Mmarekani anapojifunza lugha ngeni kama Kiswahili, na huhubiri na kufundusha. Bado atakuwa na lafudhi ya kimarekani, na namna ya Kimarekani katika kusema vitu fulani. Na mtu huyo anapohubiri au kufundisha kwa lugha isiyo yake, tofauti ya lafudhi huwavuta wasikilizaji kuwa makini kusikiliza kinachosemwa. Sawa na sisi tunapokumbana na lafudhi inayokuwa tofauti ya yetu, wakati mwingine unalazimika kusikiliza kwa umakini zaidi ili kuelewa kinachosemwa. La msingi ni kuwa, kujifunza lugha na kuongea si tu inaonyesha kuwa unajali, bali pia huwafanya watu wakusikilize!

Kwa kuhitimisha: Kila siku ninatumaini na kuiombea kazi ya Bwana, hasa hasa kazi inayoendelea katika maeneo ya huduma. Na kwa wale walioko katika maeneo ya huduma sasa, Mungu awabariki, na tunawapongeza zaidi ya mjuavyo. Na kwa wajane wote pamoja na senti zao ambazo huwezesha kazi ya huduma, Mungu awabarikini na siku moja thawabu yenu itakuwa kuu. Basi tu hawa wajane hawajui namna walivyo kwetu sisi Wamishonari.